# MAADHIMISHO YA SIKU YA DEMOKRASIA

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unaungana na watanzania wote katika kuadhimisha siku ya demokrasia duniani. Itakumbukwa kwamba siku ya demokrasia huadhimishwa kila mwaka ifikapo tarehe 15 Septemba. Siku hii maalum ilianzishwa mwaka 2007 na Mkutano mkuu wa Umoja wa Mataifa ili kuyakumbusha mataifa yote umuhimu wa kusimamia mifumo na misingi ya kidemokrasia duniani. Dhima kuu ya maadhimisho ya mwaka huu 2021 katika tafsiri isiyo rasmi ni **"Kuimarisha Uthabiti wa Kidemokrasia pindi Changamoto zinapotokea".**

Katika maadhimisho ya siku hii tunatambua umuhimu wa demokrasia, utawala bora na kuheshimu haki za binadamu katika nyanja mbalimbali ili kuhakikisha kuwa maendeleo ya taifa na watu wake yanapatikana.

Msingi wa demokrasia na haki za binadamu unatambuliwa katika matamko na mikataba mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu la mwaka 1948 na Mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala wa mwaka 2007. Pamoja na mambo mengine Mkataba wa Africa kuhusu Demokrasia katika Ibara ya 4 unazitaka nchi wanachama wa Umoja wa Africa kuhakikisha kuwa zinakuza na kulinda demokrasia, misingi ya utawala wa sheria na haki za binadamu. Ibara ya 3 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaitaja Tanzania kuwa nchi ya kidemokrasia, hivyo basi serikali inapaswa kufanya maamuzi kwa kuzingatia matakwa ya wananchi kwa ajili ya maslahi ya wananchi.

Tanzania ikiwa ni moja ya nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika, inao wajibu wa kuhakikisha kuwa haki za kidemokrasia na utawala bora zinazingatiwa. Pamoja na maboresho yanayoendelea kufanyika katika nchi yetu katika sheria na mifumo ya kidemokrasia, bado kumekua na kilio kikubwa cha wananchi na wadau wa haki za binadamu katika nyanja mbalimbali za mifumo ya kidemokrasia na utawala bora. Kwa mfano, katika kuhakikisha kuwa haki za kidemokrasia zinaheshimiwa, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania umekua ukifuatilia ushiriki wa Watetezi wa Haki za Binadamu na kuhakikisha kuwa wanashiriki kikamilifu katika michakato ya kidemokrasia nchini. Katika chaguzi za mwaka 2019 na 2020 kumekua na ushiriki mdogo wa Asasi za Kiraia katika chaguzi hizo. Kwa mfano asasi zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpigakura na kuangalia uchaguzi mwaka

2020 kwa Tanzania Bara zilikua 345 tu. Hii ni idadi ndogo ikilinganishwa na mwaka 2015 ambapo Asasi zipatazo 444 zilipatiwa nafasi ya kuangalia uchaguzi na kutoa elimu ya mpiga kura. Kutokana na ushiriki hafifu wa wananchi na wadau mbalimbali wa demokrasia nchini uchaguzi wa mwaka 2020 haukuakisi uwepo wa demokrasia makini kwa sababu Tanzania ni nchi ya vyama vingi.

Pamoja na ushiriki mdogo wa wananchi na Watetezi wa Haki za Binadamu katika chaguzi na michakato mingine ya kidemokrasia, pia kumekua na mapungufu mbalimbali katika utawala wa sheria, haki za binadamu na utawala bora.

Uwepo wa sheria zinazominya uhuru wa kujieleza, kupata taarifa na uhuru wa kujumuika zimeendelea kuwa changamoto kubwa inayochangia kukandamiza uwezekano wa wananchi kufurahia demokrasia nchini. Tumeshuhudia baadhi ya vyama vikiruhusiwa kufanya mikutano ya kisiasa wakati vyama vingine vikizuiwa kufanya mikutano. Katika Uchaguzi wa mwaka 2020, vyama vya siasa vililalamika kuhusu Uchaguzi kutokua shirikishi kwa kutozingatia misingi ya demokrasia. Kumekua na kilio kwamba matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2020 hayakuakisi sura ya demokrasia ya taifa katika mfumo wa vyama vingi. Wananchi wanategemea uwakilishi ambao unaakisi mfumo wetu. Hivyo, michakato ya kitaifa inatakiwa kua shirikishi.

Hivyo basi serikali inapaswa kuangalia misingi ya demokrasia ikiwemo ushiriki wa wananchi, uhuru wa kukutana, uhuru wa kushiriki na uhuru wa kutoa taarifa. Haki za binadamu ndiyo msingi wa demokrasia na maendeleo ya taifa lolote. Ili Taifa lolote liweze kuendelea, lazima misingi ya haki za binadamu iheshimiwwe ili kua na maendeleo endelevu.

**Wito Wetu:**

Ili kuboresha hali ya demokrasia na utawala bora nchini, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania unatoa mapendekezo yafuatayo:

i. Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ikubali kutia saini Mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda kuhusu demokrasia, ikiwemo Mkataba wa Umoja wa Afrika Kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala wa mwaka 2007.

ii. Serikali isimamie misingi ya kidemokrasia na haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, mikataba ya kikanda na kimataifa.

iii. Serikali izingatie kanuni na sheria zinazoendana na misingi ya kikatiba ili kuhakikisha kuwa utawala wa sheria unatamalaki katika nchi yetu.

iv. Serikali iweke mifumo bora itakayowezesha ushiriki wa Watetezi wa Haki za Binadamu na wananchi wote kuweza kushiriki katika chaguzi na michakato mingine ya kidemokrasia.

v. Sisi Watetezi wa Haki za Binadamu tunaamini kwa dhati kuwa maelekezo ya hivi karibuni yaliyotolewa na Mh. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu haki mbalimbali za wananchi hasa kuhusu haki za watuhumiwa na mfumo wa haki jinai nchini yatafanyiwa kazi na mamlaka husika. Hivyo tunawaomba viongozi wa mamlaka mbalimbali za serikali zikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Katiba na Sheria na idara zilizo chini yake kuhakikisha kua zinakusanya maoni ya wanachi na wadau mbalimbali ili kufanya marekebisho katika mifumo yote ya kidemokrasia na utoaji haki nchini.

vi. Serikali ya Tanzania ifikirie upya uamuzi wake wa kuzuia wananchi na mashirika yasiyo ya kiserikali kufungua kesi katika mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

vii. Serikali isikilize kilio cha wananchi wake kuhusu kukamilisha mchakato wa katiba mpya.

viii. Vyama vya Siasa vizingatie misingi ya kidemokrasia ndani ya vyama vyao wakati wote ikiwa ni pamoja na kuheshimu sheria na taratibu za vyama na nchi, uhuru wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za vyama, uhuru wa kutoa maoni na ushirikishwaji katika kutoa maamuzi.

ix. Serikali ijenge dhana ya kushauriana na kujadiliana na makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na makundi ya kidini, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla.

**Imetolewa na:-**

**Onesmo Olengurumwa,**
**Mratibu wa Kitaifa,**

**Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania**

**Dar es Salaam, Tanzania**

**15.09.2021**